



**MWAKILISHI WA KIMATAIFA KWA AJILI YA KUTOMEZA MABOMU NA
HATARI ZA VILIPUZI**

--

**UJUMBE KWA AJILI YA SIKU YA KIMATAIFA KWA AJILI YA UELEWA KUHUSU
MABOMU NA MSAADA KWA AJILI YA HATUA DHIDI YA MABOMU HAYO**

New York, 4 Aprili 2021

Nimefurahiya sana kuongeza sauti yangu leo kwa ile ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, na viongozi wengine wengi, wanaharakati, na raia wanaojali, kutoa wito kwa mataifa yote kuelekeza nguvu zao kwenye lengo la mwisho la kuondokana na ulimwengu wenye mabomu ya ardhini na mabaki ya vilipuzi vya vita. Inahitaji kuchukua uamuzi.

Tunapotoka kwenye kivuli cha janga hilo, nataka kuwasifu wanaume na wanawake ambao walishikilia mazoe na yao na kusafisha na kuharibu mamia ya maelfu yavilipuzi mwaka 2020, kuanzia mabomu ya ardhini, hadi mabomu ambayo hayajalipuka na vifaa vya milipuko. Kazi iliendelea kwa sababu watu binafsi, mashirika na serikali waliishikilia.

Uwanja mpya na salama ulijengwa nchini Kamboja, Chile ilitangaza kuwa eneo lake liko huru bila mabomu, nan chi zote wanachama wa mkataba wa kupiga marufuku mabomu zimetangaza nia yao ya kusafisha katika nchi zao mabomu ya ardhini ifikapo mwishoni mwa muongo huu.

Lakini kuna uchafuzi mpya. Mwezi uliopita tuliadhimisha miaka 10 ya vita huko Syria, mzozo ambao umesababisha mamia ya maelfu ya vifo, mamilioni wakimbizi na maelfu ya tani za uchafuzi mpya wa vilipuzi. Mapigano yanahitaji kukoma. Na usafishaji uanapaswa kuanza mapema iwezekanavyo na kwa kasi.

Na kuna uchafuzi wa zamani. Vita vya Viet Nam vilimalizika rasmi zaidi ya miaka 45 iliyopita, lakini mabomu ya ardhini na mabaki ya vilipuzi bado yanaathiri maeneo mengi.

Bomu moja la kutegwa ardhini linaweza kusambaratisha jamii: kuua baba, mama, na mara nyingi mtoto.

Dira tunayopaswa kujitahidi kuifikia ni ulimwengu ambapo watu na jamii wanaishi katika nyumba salama, kwenye viwanja salama, kwenye mazingira salama. Ambapo haki za binadamu, haki ya kuishi, uhuru, ulinzi binafsi na mahitaji ya msingi yanatimizwa na hakuna mtu yeyote aliyeachwa nyuma, wakiwemo manusura wa ajali za mlipuko, wale waliojeruhiwa na kulemazwa, ambao lazima wajumuishwe kikamilifu kama wanachama sawa wa jamii zao.

Aprili 4 ni siku ya kimataifa ya uelewa namsaada wa hatua dhidi ya mabomu, tafadhali fanya uwezalo, katika wadhifa ulionao kufikia maono haya. Heb una tuendele kuzingatia.